

Kudhibiti mashindano kwa hila ni nini?

Ni jaribio lolote la kudhibiti matokeo katika shindano ama kubadili mkondo wake wa kawaida au ya sehemu fulani tu.

Kudhibiti mashindano kwa hila kunatekelezwa kwa sababu za kufaidika kimichezo ama kifedha na wakati mwingine kupitia kwa shughuli za mchezo wa kamari ama ya bahati na sibu zilizo kinyume na sheria.

Aina mbalimbali za kudhibiti mashindano ni gani?

- Kufanya njama ya kubadili matokeo ya shindano fulani.
- Kufanya njama ya kubadili sehemu ya shindano hatua inayojulikana kama "spot fixing". Kwa mfano, kujaribu kwa makusudi ama hata kufaulu kuweka matokeo kwa njia isiyohalali katika kipindi cha mashindano.
- Kucheza chini ya uwezo wenu kwa makusudi ili kufaidika kimichezo ama kifedha kutoka kwa michezo haramu ya kamari na ile ya bahati na sibu ili kuhakikisha kwamba mtu fulani ameshinda mchezo wa kamari.
- Kutoa, kupokea ama kuomba fidia kwa matendo yoyote fisadi yanayochangia katika kudhibiti matokeo.
- Kutoa taarifa za ndani (kama vile mipango, majeraha na kadhalika) zilizo na wanariadha, maafisa na wasaidizi wao zinazoweza kutumika katika mchezo wa kamari au kufaidika kimichezo ama kifedha kinyume na maadili.

Unachopaswa kufanya ama kutofanya?

Wanariadha, Maafisa na Wasaidizi wao wanapaswa kufuata maagizo haya rahisi;

- 1 Usicheze kamari juu ya shindano lako ama juu ya shindano lolote la riadha ama juu ya mchezo wowote ulioko katika shindano lenye michezo mingi kama Olimpiki ukishiriki.
- 2 Usidhibii matokeo.
- 3 Usitoe taarifa za ndani kwa mtu yeyote. Hujui jinsi zinavyoweza kutumika.
- 4 Usikubali chochote usichostahili kama zawadi, pesa, malazi hotelini na kadhalika.
- 5 Ripoti kila wakati ukiombwa kushiriki katika shughuli zozote za kudhibiti matokeo ya shindano. Kuwa na taarifa hizi na kukosa kuziripoti kunaweza kukuletea madhara kwa kuwekewa vikwazo, kupigwa faini au hata kupigwa marufuku kabisa.
- 6 Ripoti kila wakati shughuli yoyote ya kushukiwa unayojua ukiamini kwamba ni kinyume na maadili.
- 7 Shirikiana kila wakati na uchunguzi wowote unaofanywa na Shirika la International Association of Athletics (IAAF) ama Athletics Integrity Unit (AIU)

**Ni jukumu lako kama mwanariadha kufahamu maswala ya kudhibiti matokeo katika mashindano.
Kutojua si sababu!
Kama huna hakika, wasiliana na AIU haraka iwezekanavyo**

SIMAMA IMARA, ONGEA

Unaweza kuchangia katika kupigania haki katika riadha kwa kuripoti bila kujitambulisha shughuli zozote za kudhibiti matokeo katika mashindano ama shughuli zozote za kushukiwa kwa kuandika barua pepe ukitumia anwani ifuatayo: info@athleticsintegrity.org

RIPOTI KUDHIBITI MATOKEO

Tutembelee katika Kituo cha **Athletics Integrity** kwenye mashindano ya riadha ya ulimwengu mzima yaani IAAF Athletics Championships Doha 2019